

MATUMIZI YA LUGHA YA TAMATHALI ZA SEMI KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA DIWANI YA MIDULU

Salama Salem Salama ^{1*}, Mohamed Omary Maguo ²

^{1,2} The Open University of Tanzania

*Corresponding: Omarymohamed36@gmail.com

استخدام اللغة المجازية (الصور البلاغية) في ديوان ميدولو

سلامة سالم سلامة ^{1*}، محمد عوماري ماقو ²
^{2,1} جامعة تنزانيا المفتوحة

Received: 29-03-2026; Accepted: 25-04-2026; Published: 14-05-2026

Ikisiri:

Mada ya makala haya ni kuchunguza matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika Diwani ya Midulu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Simiotiki yenye misimo ya Kihemenitiki, Kimatukio, Kiseme, Kiishara na Kiutamaduni. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Matokeo ya makala haya yamebaini matumizi ya lugha za tamathali za tashibiha, sitiari, tashihisi, jazanda na lugha isiyokuwa ya tafsida. Ufundi wa kisanaa wa kutumika kwa mbinu hizi za tamathali za semi unamfanya mtafiti kuzielewa vizuri dhamira na maudhui ambayo yamefumbatwa katika mashairi ya Diwani ya Midulu.

Maneno Makuu: Simiotiki, Tamathali za semi na Msimbo.

المخلص

يتناول هذا المقال دراسة استخدام اللغة المجازية في ديواني يا ميدولو. وقد استرشد هذا البحث بنظرية السيميائية بجوانبها التأويلية والمعرفية والدلالية والرمزية والثقافية. جمعت بيانات هذا المقال باستخدام منهج القراءة المتأنية، وحُللت باستخدام منهج التحليل الوصفي. وكشفت نتائج هذا المقال عن استخدام اللغة المجازية، كالتشبيه والاستعارة والرمزية واللغة غير التأويلية. إن البراعة الفنية في استخدام هذه التقنيات اللغوية المجازية تُسهم في فهم الباحث بشكل أفضل للقصد والمضمون الكامنين في قصائد ديواني يا ميدولو.

الكلمات المفتاحية: السيميائية، الاستعارات، والتميز.

1.1 Utangulizi

Ushairi wa Kiswahili ni utanzu ambao unasadikika kuwepo katika ulimwengu pale tu binadamu alipoanza kuwasiliana na wanadamu wenzake kwa kutumia lugha kama chombo cha mawasiliano (Chiraghdin, 1975). Ushairi wa Kiswahili ulikuwa zaidi katika kipindi cha ujio wa Waarabu katika Pwani ya Afrika ya Mashariki mnamo karne ya saba. Kuja kwa wageni hao kulisababisha kuingiliana kwa matumizi ya lugha ambapo lugha ya Kiswahili na Kiarabu ziliathiriana na pia utamaduni wa Kiarabu ukaathiriana na ule wa Waswahili. Katika mazingira hayo ushairi wa Kiswahili ukapata sura mpya ya kuwasilisha dhamira na fani ambayo inasawiri utamaduni huo mpya. Hii haina maana kuwa ushairi wa Kiswahili ndipo ulipoanzia hapo la

hasha, ushairi wa Kiswahili umekuwapo kwa miaka mingi kabla hata ya ujio wa wageni hao (Mulokozi na Sengo, 1995).

Kwa upande wake Harris (1962) na Chiraghdin (1975) wanaamini kuwa ushairi wa Kiswahili ulianza mara tu baada ya ujio wa Waarabu na kwamba asili ya ushairi wa Kiswahili ni dini ya Kiislamu na fasihi ya Kiarabu. Wanatoa kauli hii wakidai kuwa ushairi wa Kiswahili unazungumzia utamaduni wa kiarabu katika maudhui na dhamira zake na hata fani yake pia inatokana na Uarabu. Mawazo haya ni ya kweli katika muktadha wa kwamba ujio wa Waarabu ulisaidia katika kukuza fani na maudhui ya ushairi wa Kiswahili. Ushairi wa Kiswahili unatokana na shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambazo zimekuwa zikifanywa na Waswahili katika karne na karne na huimarika zaidi pale mabadiliko fulani yanapotokea katika jamii.

Shaaban Robert anatajwa kuwa ni baba wa fasihi ya Kiswahili ikiwemo ushairi ambapo ameandika kazi kadhaa ikiwa ni pamoja na *Mapenzi Bora* diwani ambayo inasaidifu mambo mbalimbali si ya jamii ya Waswahili tu bali jamii mbalimbali duniani (Njogu na Chimera, 1999). Washairi wengine waliofuata nyayo za Shaaban Robert katika kutunga mashairi ni Saadan Kandoro, Mathias Mnyampala, Jumanne Mayoka, Salim Kibao, Sudi Andanenga na wengine (Omary, 2011). Baada ya hapo wamekuja washairi wengine wengi ikiwemo Tigiti Shaaban Yusuf Mnyagatwa Sengo ambaye ameandika diwani kadhaa za mashairi ikiwemo hii ya *Diwani ya Midulu* aliyoiandika mwaka 2010. Diwani hii inaelezea masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Watalaamu kadhaa wamevutiwa na mashairi ya diwani hii hata kuandika makala na kufanya utafiti juu ya diwani hii. Safari (2010) aliandika utangulizi wa diwani hii na kufanikiwa kuchambua baadhi ya mashairi. Katika maelezo yake anaeleza kuwa diwani hii inaeleza juu ya umuhimu wa kudumisha utu wa binadamu katika maisha kwa kuwa hapa duniani ni mahali tu pa kupita na maisha mazuri yapo Peponi. Maisha hayo ya Peponi yatapatikana kwa mja ambaye amekuwa akitenda matendo ya kiutu katika maisha yake. Maelezo haya tunakubaliana nayo ndiyo maana tukaona kufanya utafiti na kuandika makala haya ili kubaini fani iliyotumika katika diwani hiyo.

August (2016) aliandika juu ya usawiri wa nafasi ya mwanamke katika mashairi yanayopatikana katika *Diwani ya Midulu*. Katika maelezo yake anabainisha kuwa ndani ya diwani hiyo mwanamke anasawiriwa kama mama mlezi, kiumbe mwenye upendo, mvumilivu, mtunza siri na mwenye heshima. Usawiri huu wa mwanamke katika diwani hiyo una uhalisia katika maisha ya kila siku kwani mwanamke amekuwa ni mlezi wa familia wakati mwingine katika mazingiza magumu. Baadhi ya wanawake huwa hawana waume na hivyo kulazimika kulea watoto wao. Kufahamu kuwa diwani hii inazungumzia utu kama dhamira kuu kumetuvutia kuchunguza fani ya diwani hiyo.

Fani ni ufundi wa kisanaa ambao mwandishi anautumia katika kazi yake kwa lengo la kuipamba kazi hiyo ili ipendwe na wasomaji. Katika kutazama fani ya kazi ya fasihi mhakiki huukiliwa na vipengele mbalimbali kama vile muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wakati, uteuzi wa maneno, tamathali za semi, misemo, methali, mandhari na wahusika (Wamitila, 2002). Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya tamathali za semi katika *Diwani ya Midulu* kwa kurejelea vipengele tashibiha, sitiari, tashihisi, **jazanda na matumizi ya lugha isiyokuwa tafsida kama sehemu ya vipengele vya fani ili kufanikisha lengo kuu la makala haya.**

Hivyo basi kutokana na usuli wa makala haya tatizo la utafiti ambalo limetusukuma kuandaa makala haya ni kutaka kuweka bayana matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika Diwani ya Midulu ili kuweka wazi dhamira zinazojengwa kupitia tamathali hizo na kuwafikia wasomaji kwa namna ambayo inaeleweka zaidi kwao. Hii pia itakuwa ni faida kubwa kwa wanajamii na hadhira ya diwani husika kufahamu maudhui yaliyopo katika diwani husika. Lengo la makala haya ni kuchunguza matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika ushairi

wa Kiswahili huku mifano ikiwa ni kutoka katika diwani teule ya Midulu. Diwani hii imeandikwa na Tigiti Sengo na kuchapishwa mwaka 2010 nchini Tanzania.

2.1 Mkabala wa Kinadharia

Mkabala wa kinadharia hurejelea nadharia ambayo imetumika katika kuchambua data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma. Nadharia ni muongozo ambao unaeleza namna kitu au jambo fulani linavyotakiwa kuwa au linavyotakiwa kufanywa ili kutimiza lengo kuu la utafiti husika. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Simiotiki katika kuchambua data za utafiti.

2.1.1 Nadharia ya Simiotiki

Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Simiotiki iliyoasisiwa na mtaalamu Ferdinand Dissuessa ikiwa na mikondo mbalimbali kama vile Simiotiki na Naratolojia. Simiotiki ni nadharia ambayo inaeleza kuwa lugha inayotumika katika kazi za fasihi ni lugha ambayo imeundwa kutokana na sauti za lugha na kunasibishwa kimaana ili watumiaji wa lugha husika waweze kuelewana (Chao, 1968). Pamoja na kunasibishwa pia lugha hutumika kiishara katika kuwasilisha maana mbalimbali kwa wazungumzaji wake.

Mtaalamu huyu anaeleza kuwa katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni vitaja na vitajwa. Vitaja ni majina ambayo yanataja vitu fulani na vitajwa ndiyo hivyo vinavyotajwa na majina hayo. Kwa mfano neno “nyumba” ni kitaja ambacho kinarejelea kitajwa ambacho ni kitu halisi ikiwa ni nyumba ambayo watu wanaishi ikiwa na vyumba vya kulala na sebule ya kupumzikia. Hii yote inaonyesha namna binadamu alivyokuwa na uwezo mkubwa wa kubuni na kuunda lugha yake ili aweze kuitumia kwa namna ambayo itamsaidia katika mawasiliano.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa ukitaka kuifahamu nadharia ya Simiotiki katika kazi za fasihi tazama namna inavyotumika katika kuunda vipengele kama vile muundo, mtindo, matumizi ya lugha, ujangaji wa wahusika na mandhari. Vipengele hivi vyote vinajengwa kwa muundo maalumu na havipo kiholela katika fasihi. Tunapomuona mwandishi ameamua kuwa na wahusika wa aina fulani hapo ni muundo fulani unakuwa umetumika. Kwa mfano Shaaban Robert katika anatumia wahusika ambao wanafahamika kama wahusika bapa ambao wanakuwa na aina moja ya tabia katika matukio yao yote wanayoyafanya au kuwakumba wanapokuwa katika riwaya husika. Huu ni muundo wa wahusika katika riwaya za mtunzi huyu lakini watunzi wengine wanaweza kuwa na muundo tofauti (Wamitila, 2008). Matumizi ya muundo huo wa wahusika unasaidia sana katika kujenga misimbo ambayo humsaidia msomaji kuipata dhamira ya mtunzi wa kazi ta fasihi.

Katika fani ya ushairi tunakuwa na vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha ikiwemo tamathali za semi (Mulokozi, 1996). Nadharia hii imetufaa katika utafiti wetu kwa sababu fani ni ufundi wa kisanaa ambao unatumiwa na mwandishi katika kuisana kazi yake (Njogu na Chimerah, 1999). Ufundi unaosemwa hapa ni ule ujuzi wa kuunda vipengele mbalimbali vya fani katika kazi ya fasihi. Hivyo kwa kutumia nadharia hii tumeweza kuchambua matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika *Diwani ya Midulu* kwa kurejelea misimbo ya nadharia ya Simiotiki ambayo ni msimbo wa Kihemenitiki, Kiishara, kiseme, kimatukio na kiutamaduni (Barthes, 1994).

Msimbo wa Kihemenitiki huu hujengwa katika mada au kichwa cha kazi ya fasihi na msomaji anaposoma tu kichwa hicho mara moja huelewa dhamira zilizokusudiwa na mtunzi (Deacon, 1997). Kwa mfano, msomaji anapokutana na jina la kitabu *Mashetani* mara moja ataanza kujenga dhamira ambazo anahisi kuwa zinapatikana ndani ya kazi husika. Msimbo huu tumeutumia katika utafiti wetu hasa kwa kutazama vichwa vya mashairi na kutusaidia kufahamu dhamira ambazo mtunzi amezijenga ndani ya shairi.

Msimbo wa kiseme hutokea pale mtunzi anapokuwa anatumia maneno fulani yenye maana kisemantiki lakini maana ya msingi ya neno husika inanasibishwa na maana nyingine za ziada za kifasihi kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa hadhira yake (Deely, 1990). Mtunzi wa kazi ya fasihi huweza kutumia neno kama vile “simba” na kulipatia maana nasibishi nyingi kuwa mtu ni mkali sana au ni mkorofi. Katika kazi za fasihi ni jambo la kawaida kukuta mhusika

aliyepewa jina la simba na yale ambayo anayafanya yana mnasaba mkubwa na tabia na matendo ya mnyama simba.

Msimbo wa kimatukio nao pia umetumika katika utafiti wetu ambapo msimbo huu hujitokeza pale ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi anapounda tukio kwa njia ya msimbo ambao unawakilisha kitu fulani (Eco, 1984). Katika kazi ya fasihi kunaweza kuwa na tukio la mnyama kama “mbwa” akiwa anatenda kitendo cha kudokoa nyama au kitu kingine na kula kwa ulafi. Tukio hili linakuwa limeandaliwa makusudi kwa ajili kuonesha tabia ya watu ambao ni walafi na wana tamaa katika maisha yao. Tukio hilo linaweza kuwa ni mahususi kwa ajili ya kuonesha uongozi mbaya katika jamii.

Utamaduni ni jumla ya mambo yote katika maisha ya binadamu na kupitia utamaduni kunajengwa misimbo ya aina mbalimbali (Frutiger, 1984). Jamii hufanya masuala mengi ya kiutamaduni ikiwa ni pamoja na sherehe, misiba, ibada, michezo na mambo mengine yenye kuhusiana na hayo. Katika matukio haya kunajengwa misimbo ya aina kwa aina na mfano mzuri ni kitabu cha “Arusi ya Buldoza na Hadithi nyingine,” cha mtunzi Said Ahmed Mohamed Khamis. Tayari katika jina la kitabu kunajengwa msimbo wa kiutamaduni na msomaji atazielewa vizuri dhamira za kitabu hicho baada ya kuufafanua vizuri msimbo huu wa kiutamaduni.

Msimbo wa mwisho ni ule wa kiurejelezi au kiishara ambapo huu hujitokeza kutokana na kutajwa kitu ambacho kwacho urejelezi hufanywa (Hoffmeyer, 1996). Kwa mfano, msomaji anaposoma au kusikiliza kazi ya fasihi na kukutana na neno “mrembo” mara moja hupata ishara na urejelezi juu ya huyo mrembo. Msomaji hupata picha kuwa mrembo huyo atakuwa ni mzuri wa sura au umbo, mrefu, na mwenye nywele nzuri na sifa nyingine nyingi atakuwa nazo kichwani kwake.

Kwa hakika, nadharia ya Simiotiki imetumika katika kuchambua matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika *Diwani ya Midulu* na imezeshia kutimiza lengo la makala. Nadharia hii imekuwa ni faafu katika utafiti huu kwa sababu kwa asili yake ni nadharia ambayo inahusiana na masuala ya uchambuzi wa lugha kwa kurejelea misimbo mbalimbali. Tamathali za semi hujengwa kupitia picha, balagha, ishara, taswira na mafumbo na hivyo nadharia hii ni muafaka katika kuchambua data za makala haya.

3.1 Methodolojia ya Makala

Sampuli ya makala haya ilikuwa ni kitabu kimoja cha mashairi ambacho ni *Diwani ya Midulu* na kimeteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Data za makala haya zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kwa kusoma mashairi yaliyopo katika *Diwani ya Midulu*. Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kusoma kwa makini matini iliyoteuliwa kwa ajili ya kutoa data za utafiti (Kothari, 2008).

Katika kukusanya data kwa kutumia mbinu hii alizingatia zifuatazo: Hatua ya kwanza ilikuwa ni kusoma mashairi ya diwani husika zaidi ya mara tano bila kudondoa chochote ili kupata uelewa wa jumla kuhusu fani iliyotumika katika diwani teule. Hatua ya pili ilikuwa ni kuweka mada ambazo data za utafiti zikusanywa ili kuendana na madhumuni ya makala. Hatua ya tatu ilikuwa ni kusoma mashairi ya kudondoa maneno, mshororo au ubeti ambao una matumizi ya kipengele cha fani. Hatua ya nne ilikuwa ni kuweka pamoja vipengele vya fani vinavyofanana kutoka katika mashairi mbalimbali ili kuepuka marudio na hatua ya nne ilikuwa ni kusoma na kuziweka data katika namna rahisi ya kuzichambua ili kutimiza lengo la makala haya.

Data za makala haya zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ni muafaka katika utafiti huu kwani ni mbinu inayotumika kuwezesha kutolewa kwa maelezo ya kiuchambuzi ambayo yanatoa tafsiri ya data za utafiti (Kombo na Tromph, 2009).

4.1 Matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika *Diwani ya Midulu*

Fani katika fasihi huelezwa kuwa ni ufundi na ubunifu ambao umetumika katika kazi ya fasihi na kuifanya kuweza kufikisha ujumbe kwa hadhira yake kwa nzuri ambayo inakubalika katika jamii husika (Njogu na Chimera, 1999). Matumizi ya lugha ni sehemu ya fani katika kazi ya fasihi ambayo inachukua nafasi kubwa wakati mwingine kuliko vipengele vingine vya fani. Tamathali za semi ndicho kipengele kipana katika lugha ya kifasihi na hususani katika mashairi. Hii ni kwa sababu mashairi yanatumia lugha ya mkato na ufupisho na hivyo tamathali za usemi ndio mahala pake hasa katika mashairi.

4.2.1 Tashibiha

Tashibiha ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha na kuvifaninisha vitu viwili kuwa vinafanana kwa kutumia lugha ya “mithili ya yaani mfano wa, kama, ja, japokuwa, sawasawa na, sawa kabisa na, anafanana kama, kinafanana kama, mfano wake,” nakadhalika (Wamitila, 2008). Tamathali hii ya semi hutumika katika mashairi ambapo mashairi hutumia tashibiha moja kuwasilisha dhamira nyingi kwa hadhira yake. Katika *Diwani ya Midulu* tumeona matumizi ya tashibiha yakijitokeza katika mashairi mbalimbali kama shairi la “Bwana Miti Kazi Zake,” ambalo tumedondoa sehemu ya beti zake hapa chini:

...

4. Kakaliya kuti kavu, mwenyewe hata hajuwi
Roho yake ni chakavu, mwilini aumwa ndui
Kaunguwa kawa jivu, makucha yake ja chui
Bwana miti kazi zake

5. Kuvichokoza viwavi, miguuni ni siyafu
Hajuwi “cha mtu mavi” hakunalo yai bofu
Kumbe lenyewe ni bavi, joshole maji machafu
... (Uk. 115).

Hapa tumedondoa ubeti wa nne na wa tano ambapo tunaona kuna matumizi ya tashibiha. Ubeti wa nne katika mshororo wa tatu unaeleza kuwa, “Kaunguwa kawa jivu, makucha yake ja chui,” ambayo ni tashibiha yenye kumfananisha bwana miti na mnyama chui. Hapa kunajengwa dhamira juu ya utunzaji mbaya wa miti na misitu kwa jumla. Afisa misitu ambaye kucha zake zinafaninishwa na mnyama chui maana yake ni kuwa, badala ya yeye kuwa ni mtu makini katika utunzaji wa misitu lakini yeye ndiye tena ambaye anafanya kazi ya kuharibu misitu. Hili hufanyika kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa vibali ambavyo si halali na wakati mwingine kupokea rushwa kutoka kwa wananchi. Chui ni mnyama mkali sana na kucha zake ni kali kiasi cha kumrarua adui yake na kumuua. Afisa misitu ambaye anafaninishwa na kucha za chui ni mtu ambaye kwa vyovyote vile hana maadili katika kazi yake na anahatarisha usalama wa misitu. Haya yanajibainisha katika mshororo wa tatu wa ubeti wa wa tano hapo juu, ambapo inasemwa, “Kumbe lenyewe ni bavi, joshole maji machafu.” Jasho la afisa misitu kufaninishwa na maji machafu ni ishara ya kuwa mtaalamu huyo hana maadili kabisa katika utendaji kazi wake. Maji machafu ni kitu ambacho hakithaminiwi kabisa katika jamii kwa sababu huweza kusababisha matatizo ya kiafya kwa wanajamii. Kuona kiongozi au mtumishi wa umma ambaye anafaninishwa na maji machafu maana yake ni kuwa kiongozi huyo hafai kabisa kuwa mtumishi au kiongozi wa umma (Sengo, 1973a; 1973b).

Matumizi mengine ya tashibiha tunayapata katika shairi la “Watangulizi,” katika ubeti wa 2 ambao umedondolewa hapa chini:

...

Kwa KUN ya Muumbizi, Adamu aliumbika
Kwa ya pili ja andazi, na Hawa akafanyika
Vitazameni viyazi, wote hawakuzalika
Mambo ni kumithilika, kifo sawa usingizi

Katika dondoo hili, kifo kinafananishwa kuwa ni sawa na usingizi. Mtu anapokuwa amelala ni sawasawa na mtu huyo kuwa amekufa kwa sababu anapokuwa ndani ya usingizi anakuwa hana ufahamu kama anapokuwa hayuko katika usingizi. Haya yanajibainisha katika mshororo wa mwisho “Mambo ni kumithilika, kifo sawa usingizi.” Kwa mujibu wa mafundisho ya dini ya Kiislamu ambayo mtunzi wa *Diwani ya Midulu* anasisitiza sana ni kwamba ni vizuri kila binadamu akatafakari kifo kupitia usingizi. Hii inaweza kumfanya kuwa mcha Mungu kwa kuamini kwamba kifo kinaweza kuja saa yoyote ile kama usingizi unavyokuja saa yoyote. Kwa kulifahamu hilo itakuwa ni jambo jema kwa kila mtu kufanya mambo mema ili saa yoyote kifo kikimkuta basi kimkute akiwa na matendo mema mengi aliyoyafanya. Matumizi mengine ya methali yanapatikana katika shairi la “Kichwa kikichoka kazi,” katika ubeti wa pili mshairi anasema:

...

Maisha ni kama nazi, huna hakika na tuwi
Lini takwisha pumzi, siku hini huijuwi
Saa zote usingizi, bega ja kichwa haliwi
Kiza mara hakikawi, kichwa kikichoka kazi

Tashibiha inapatikana katika mshororo wa kwanza usemao, “Maisha ni kama nazi, huna hakika na tuwi,” ambapo ni sawa na kusema kuwa maisha ni kitu ambacho wakati mwingine hakitabiriki. Katika maisha, wanadamu hupanga mambo mengi lakini yale wanayofanikiwa kuyakamilisha huwa ni machache na siyo yote. Hii inaonyesha kuwa, maisha ni kama ilivyo kwa nazi ambapo ukiiona kwa nje unaweza kudhani ndani ikawa vizuri kumbe ni koroma ambalo haliwezi kutoa tui. Katika maisha na kupata na kukosa na hivyo ni vema kila mtu akalifahamu hili ili kuwa na amani ya moyo katika maisha ya kila siku. Matumizi mengine ya tashibiha tunayaona katika shairi la “Mgeni ni Mtu gani?” katika ubeti wa saba kuwa:

...

Mgeni kudhalilishwa, kama kawa siniyani
Wengine hufurahishwa, wakiwawo ugenini
Busara kutotapishwa, hekima za safarini
Mgeni ni mtu gani, tunaomba kujulishwa.

Mshoro wa kwanza ndio ambao una matumizi ya tashibiha ambayo inamfananisha mgeni na “kawa” ambacho ni kifaa kinachotumika katika kufunika chakula au wakati mwingine kama pambo katika nyumba. Kinachosemwa hapa ni kuwa, katika baadhi ya mazingira mgeni anaweza kufika kwa wenyeji wake halafu asihudumiwe wala kutiliwa maanani kama ilivyo kwa “kawa” ambalo hutumika kufunika chakula na hali ya kuwa kawa hilo halifaidi chochote katika chakula husika. Wanaofaidi ni wengine na sio kawa, jambo hili linaweza kuwa na mantiki kubwa pale ambapo mgeni anaweza kuwa ni tegemeo kubwa la maisha kwa wenyeji wake lakini wenyeji hao wasimjali na kumpa thamani anayostahili.

Matumizi ya tashibiha katika *Diwani ya Midulu* yanaonekana kuwa na uzuri ambao unaonekana bayana kutokana na mtunzi kuunda tashibiha zake kutokana na mazingira ambayo yanaizunguka hadhira. Hii inamfanya msomaji kuwa na uwezo wa kujenga dhamira mbalimbali tena kwa haraka sana. Tashibiha hizi zinaweza kueleweka hata kwa hadhira yoyote ile na sio lazima iwe ni ya kiwango cha juu katika upevu wa mashairi. Hii ni diwani nzuri kwa wale ambao wanapenda kujifunza kuchambua mashairi kwa kuwa watakutana na tashibiha ambazo zinatokana na maisha yao ya kila siku na hatimaye kuweza kuibua dhamira (Hawkes, 1977). Sasa tutazame matumizi ya sitiari katika diwani teule ambayo ni *Diwani ya Midulu*.

4.1.2 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya semi ambayo hutumika kulinganisha vitu viwili kwa kutumia viunganishi na hasa kiunganishi “ni,” kwa kuvifanya vitu hivyo kuwa ni sawasawa kabisa na hakuna tofauti yoyote ya msingi baina ya vitu hivyo (Hoffmeyer, 1996). Sitiari hujitokeza katika mazingira

kama vile, Mwanaidi ni chui, maharage haya ni sukari, kuimba ni utajiri na Joyce ni sungura. Sitiari ni tamathali ya semi ambayo inatumika kwa kiwango kikubwa katika kazi za fasihi na hasa mashairi kutokana na ule uwezo wake kubeba dhamira kuntu ndani yake. Ligembe (1995) anaeleza kuwa, ukisoma kazi ya fasihi kwa makini utabaini kuwa karibu kila kitu ni sitiari kutokana na ukweli kwamba, sitiari ndiyo ambayo ina uwezo mkubwa wa kubeba dhamira nyingi kwa mara moja. Katika *Diwani ya Midulu* kuna matumizi ya sitiari katika mashairi mbalimbali na hapa tunaanza na shairi la “Wanisema ni Mkali,” katika ubeti wa tatu na wa nne kwamba:

...

Uso wako ni kufuli, kwa wiki na usununi
Mitihani ulifeli, wauza nini mwilini
Bara ujali ubali, ukajificha konani
Mtafiti firauni, mambo yaliyomfeli
Sura yako ya tumbili, bora ungekuwa nyani
Matusiyo sihimili, ingawa moyo makini
Nakufunza somo hili, acha kuchukia dini
Utapoingiya mavani, itakutoka fedhuli (uk. 122).

Sitiari ya kwanza inapatikana kupitia mshororo wa kwanza usemao, “Uso wako ni kufuli, kwa wiki na usununi.” Uso unafananishwa na kufuli si jambo la kawaida lakini hapa tunaielezwa kwamba uso unafananana kabisa na kufuli na hakuna tofauti yoyote. Kifasihi, kinachobainika hapa ni kwamba, mtu huyo ambaye uso wake unafananishwa na kufuli ni kwamba ni mtu ambaye hana tabasamu na ni mtu mwenye roho mbaya ambayo haisemekiki katika jamii yake. Msimbo wa Kiurejelezi ndio ambao unatusaidia kuelewa dhamira ambayo inawasilishwa hapa kuwa ni mtu katili ambaye akishaamua jambo lake ni vigumu kubadili msimamo wake (Frutiger, 1989). Pia, ni mtu ambaye hana huruma ya aina yoyote ile na anaweza hata kuua au kumdhuru mtu. Ni mtu ambaye hana aibu anaweza kufanya jambo lolote baya katika jamii bila woga wala wasiwasi wowote. Katika ubeti huohuo inatajwa kuwa mtu huyo anafanya biashara ya kuuza mwili wake, yaani kahaba. Katika mazingira ya kawaida mtu kuamua kufanya biashara ya ukahaba ni lazima mtu huyo awe ameondoa aibu yote kwa sababu sio jambo ambalo linakubalika katika misingi ya dini na utamaduni wa jamii. Kulifanya jambo hilo ni lazima “uso uwe umefungwa kwa kufuli.” Hapa pia tumesaidiwa na msimbo wa kiutamaduni ndipo tukaweza kuielewa vizuri dhamira lengwa ya masuala ya ukahaba na aibu.

Katika ubeti wa nne pia tunaona matumizi ya sitiari, “Sura yako ya tumbili, bora ungekuwa nyani.” Hapa sura ya binadamu inafananishwa kuwa ni sawasawa kabisa na ya tumbili. Tumbili ni mnyama ambaye huwa ni mjanja sana wakati mwingine kumzidi nyani. Binadamu ambaye anatajwa kuwa na sura hii huwa ni mtu ambaye haaminiki katika kauli zake na ahadi zake kwa sababu hudanganya sana. Watu wa aina hii wapo katika jamii na husababisha matatizo mengi kutokana na tabia yao ya utapeli. Matumizi mengine ya sitiari tunayaona katika shairi la “Nilikwambiwa Kitambo,” katika ubeti wa nne kwamba:

...

Hata unapoteleza, watajua kujikwaa
Ogopa kuwapuuza, jihifadhi ukikaa
Jifanye kama ajuzi, maishani uwe taa
Wakuone wawafaa, ogopa kuwachukiza

Kitendo cha binadamu kufananishwa na “taa” ni sitiari nzuri sana ambayo inamchora binadamu kama mtu ambaye ni kiongozi katika jamii na anaweza kutoa muongozo mzuri kwa watu wake wa karibu na jamii kwa jumla. Suala la binadamu kuepuka kujikweza ni la muhimu sana kwani ni kupitia jambo hilo ndipo watu watampenda binadamu huyo na kumfanya kuwa kiongozi wao wa mfano. “Taa” ndiyo imulikayo mahali palipokuwa na giza pakawa na mwanga na pale pasipokuwa na njia pakawa na njia. Hivyo, binadamu anapaswa kuishi katika maisha yake ya

kila siku akijipa nafasi ya taa akitambua kuwa wapo watu nyuma yake ambao wanamtazama yeye kama mfano. Wapo baadhi ya watu ambao hawautambui ukweli huu wamekuwa wakifanya mambo ya ajabu sana ambayo hayafai kuigwa na huyafanya tena mbele ya watoto wao. Kwa mfano, unakutana na mzazi ambaye ni mlevi wa kupindukia ambaye kila siku hurejea nyumbani akiwa amelewa. Watoto wake wanajifunza nini kutoka kwa mzazi huyo? Hapa kwa hakika wanachojifunza ni kitu kibaya ambacho pengine kinaweza kuwafanya kuwa na tabia zisizokubalika katika jamii ikiwa ni pamoja na ulevi.

4.2.3 Matumizi ya Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya semi ambayo huvipa vitu visivyokuwa na urari wa kibinadamu kutenda kama binadamu (Sengo, 1987). Kimsingi, katika hali ya kawaida huwa sio rahisi kuona au kisikia jiwe likizungumza au likicheka lakini katika ulimwengu wa fasihi na hasa fasihi simulizi ni kawaida kabisa kuona hayo yakitokea. Katika *Diwani ya Midulu* tumeona kuna matumizi ya tashihisi katika mashairi kadhaa na hapa tumetoa mfano kupitia shairi la “Ufisidi Ufisadi kama ifuatavyo:

Masikini Tanzaniya, nchi inakamuliwa
Watu wake wenye niya, leo wanasumbuliwa
Wazawa mamiyamiya, tosini wanakaliwa
Lini watatambuliwa, haqi kuzisimamiya? (uk. 148).

Katika mshororo wa kwanza kipande cha pili ndiko kwenye matumizi ya tashihisi isemayo, “Masikini Tanzaniya, nchi inakamuliwa.” Katika hali ya kawaida kinachokamuliwa huwa ni maziwa ya ng’ombe, mbuzi, ngamiya na wanyama wengine. Pia, mafuta ya aina kadhaa ya kupikia hupatikana baada ya mbegu husika kukamuliwa katika mashine muafaka lakini hapa inaelezwa kuwa kinachokamuliwa ni nchi. Hii kwa hakika ni tashihisi ambayo inaeleza juu ya rasilimali za nchi kama madini na vitu vingine vinachukuliwa na wageni ambao wanaitwa wawekezaji kwa manufaa yao wao wenyewe. Nchi inaachwa bila ya kupata faida ya aina yoyote ile na kuendelea kuwa masikini. Hili kwa hakika ni jambo ambalo halikubaliki hata mara moja na ndio maana serikali ya Tanzania imefanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinatumika vizuri kwa manufaa ya wananchi wote na sio wachache tu. Kupitia nadharia ya Simiotiki na msimbo wake wa kimatukio tumeweza kufahamu kuwa kitendo cha nchi kukamuliwa ni tashihisi ambayo inaelekeza juu ya kunyonywa kwa rasilimali za nchi na kweli zimekuwa zikinyonywa (Deely, 1980). Rasilimali za taifa zimekuwa zikinyonywa si tu na wawekezaji bali pia baadhi ya viongozi ambao wakekuwa sio waadilifu. Serikali ya Tanzania imepambana na hali hiyo na bado inaendelea kupambana nayo kiasi hata cha kufungua mahakama maalumu kwa ajili ya mafisadi.

Matumizi mengine ya tashihisi tunayoana katika shairi la “Nilikwambiya Kitambo,” katika ubeti wa kwanza kwamba:

Kuna ukubwa ukuza, mwili mtambo mtambo
Kuwanda kunapendeza, hasa wapenda vitambi
Hata ukiwauliza, huyapapasa matumbo
Nilikwambiya kitambo, malezi yatakuuza (uk. 161).

Matumizi ya tashihisi yanajitokeza katika mshororo wa mwisho kwamba, “Nilikwambiya kitambo, malezi yatakuuza,” ambapo malezi yamepewa uwezo wa kuuza. Katika biashara ndiko ambapo binadamu anaweza kuuza na kununua bidhaa mbalimbali lakini malezi hayana uwezo wa kuuza au kununua kitu. Hata hivyo, jambo la msingi linalosemwa hapa ni kwamba, malezi kwa watoto ni jambo jema sana kwa sababu malezi ndiyo ambayo yatamfanya mtoto kuwa na nidhamu au la, na kisha kukubalika au kutokubalika katika jamii yake. Mtu ambaye amefanikiwa kupata malezi mazuri mambo yake huwa ni mazuri kila siku ikilinganishwa na yule ambaye hakupata malezi mazuri. Hata katika suala la kuoza tu, watu hupenda kuoza au kuolewa na mtu mwenye tabia nzuri. Mara nyingi uzuri wa sura sio jambo la msingi sana

linalotazamwa wakati wa posa zaidi malezi na tabia ya mhusika ndivyo ambavyo hupewa kipaombe (Sengo, 2009; Massoud, 2022).

4.2.4 Matumizi ya Jazanda

Jazanda ni tamathali ya semi ambayo kwa kawaida hulinganisha vitu viwili bila kutumia viunganishi (Acquaviva, 2004; Wamitila, 2008). Hii inaweza kuonekana katika jazanda kama “elimu bahari, mtu afya, maji marefu nakadhalika. Katika kazi za fasihi huwa kunakuwa na matumizi ya jazanda na mfano mzuri ni katika *Diwani ya Midulu* katika shairi la “Wapendwapendwa ni Mngu,” katika ubeti wa 3 anasema:

Anahimiza mazuri, naye huishi vizuri
Anaogopa kiburi, akihofu ya kaburi
Kamwe yeye si jeuri, kwa kumchawe kahari
Yeye mtu wa saburi, ulimi wake sukari

Matumizi ya jazanda yanajibainisha vizuri katika mshororo wa mwisho kama unavyosomeka “Yeye mtu wa saburi, ulimi wake sukari.” Katika hali ya kawaida ulimi wa binadamu hauwezi kuwa sukari lakini hapa kinachorejelewa ni maneno ya hekima na yenye adili yatokayo kwa mtu huyo ambaye hakutajwa bayana katika shairi. Ulimi wenye sukari ndio unaofaa katika kutoa malezi mema kwa jamii. Itakuwa ni jambo la ajabu sana kuona mzazi akiwa anazungumza au anawaelekeza watoto wake kwa lugha ya matusi na kejeli badala ya kutumia lugha nzuri zaidi. Ulimi ndio ambao hujenga au kubomoa mambo katika jamii kwani jambo lolote lile huanza katika mipango na baadaye kuhamia katika utakelezaji. Ni maneno ndiyo ambayo hutumika katika kupanga mipango lakini pia ni maneno hayohayo ambayo hutumika katika kuwezesha utekelezaji wa mipango husika. Kwa hakika hakuna mradi au mpango wowote wa maendeleo ambao umewahi kufanikiwa duniani bila ya mawasiliano. Mawasiliano ndio msingi wa maendeleo yoyote yale katika jamii. Kwa kutumia msimbo wa kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki tunapata kuelewa kuwa “ulimi,” ndio msingi wa kila kitu katika maisha ya binadamu (Deacon, 1997; Kisarazo, Maguo & Mahonge, 2025). Ikiwa ni katika matibabu, elimu, siasa, biashara, kilimo, ufugaji, amani, ulinzi na usalama ni ulimi ndio ambao unafanya kila kitu kiende sawa na kuwa vile kilivyo au kinavyotakiwa kuwa. Sasa tuone matumizi ya lugha isiyokuwa ya tafsida katika *Diwani ya Midulu* kama ifuatavyo:

4.2.5 Lugha Isiyokuwa ya Tafsida

Lugha ya tafsida ni ile ambayo inapotumika vitu ambavyo havipaswi kuelezwa kwa lugha ya wazi huelezwa kwa lugha ya tafsida (Wendo & Titus, 2025). Pia, ni vema ikaeleweka kuwa katika hali ya kawaida tafsida hutumiwa kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno ambayo kimsingi yalipaswa kutamkwa katika faragha au lugha ya staha pale yanapotajwa katika mazingira ya bayana yasiyokuwa ya faragha. Matumizi ya lugha isiyokuwa ya tafsida katika *Diwani ya Midulu* yanapatikana katika shairi la “Watu Wasio Khisani,” lililopo katika ukurasa wa 121 katika ubeti wa tatu:

...
Yote aliyotendewa, kayatupa jalalani
Hakumbuki kafanyiwa, hakiri kuna Hanani
Hunuka kama kanyewa, hana moja la thamani
Watu waso ikhisani, hakuna walizaliwa.
...

Mshororo wa tatu katika ubeti huu hususani kipande cha kwanza kina matumizi ya lugha isiyokuwa ya tafsida kwamba, “hunuka kama kanyewa.” Kwa hakika lugha hii sio ya tafsida kwani imetaja jambo ambalo kwa mujibu wa mila na desturi huwa halitajwi waziwazi. Matumizi ya lugha hii isiyokuwa ya tafsida mara nyingi huifanya kazi kuonekana kwamba imekiuka mila na desturi za jamii husika. Hata hivyo, lengo la kutumia lugha ya aina hii ni kutaka kufikisha ujumbe kwa hadhira kwamba, mtu asiyekuwa na shukurani kwa jambo lolote alilofanyiwa na mtu au watu wengine ni mtu mbaya sana na inatakiwa aelimishwe vya kutosha

ili kuepukana na hali au tabia hiyo. Kwa kutumia misimbo ya kiseme na kiutamaduni ya nadharia ya Simiotiki tumeona kwamba, neno “kunyewa,” ambalo limetumika linakiuka taratibu za mila na desturi ambapo maneno kama vile “haja kubwa,” ndilo lililokuwa ni muafaka zaidi. Inapasa kutumia lugha ya tafsida katika maandishi ili kuepuka kukiuka maadili na miiko ya jamii husika.

4.2 Hitimisho

Makala haya yameangazia matumizi ya lugha ya tamthali za semi katika *Diwani ya Midulu* na kufanikiwa kubainisha vipengele vitano ambavyo ni tashibiha, sitiari, tashihisi, jazanda na lugha isiyokuwa ya tafsida. Kupitia vipengele hivi vya matumizi ya lugha diwani ya Midulu imeweza kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Ufundi wa kisanaa uliotumika katika mbinu hizo unadhihirisha kwamba ushairi wa Kiswahili ni chombo muhimu katika kujenga jamii kwa kuipatia dhamira na maudhui kwa njia ya kisanaa.

MAREJELEO

- Acquaviva, G. (2004) “Jazanda ya Njozi katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi,” *Katika Swahili Forum na. 11: 69-73.*
- August, K. F. (2016) “Kuchunguza taswira ya Mwanamke katika Mashairi ya Tigiti Sengo: Mfano wa Diwani ya Midulu.” *Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*
- Barthes, R. (1994) *The Semiotic Challenge.* Berkely: University of California Press.
- Chao, Y. R. (1968) *Language and Symbolic Systems.* Cambridge: Cambridge University Press.
- Chiraghdin, S. (1975) “Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili,” katika *Mulika na. 7,* Dar es Salaam: TUKI.
- Deacon, T. W. (1997) *The Symbolic Species: The Co-Evolution of Language and the Brain.* New York: Norton.
- Deely, J. (1990) *Basics of Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.
- Eco, U. (1984) *Semiotics and the Philosophy of Language.* Bloomington: Indiana University Press.
- Frutiger, A. (1989) *Signs and Symbols.* New York: Van Nostrand.
- Harris, L. (1962) *Swahili Poetry.* London: OUP.
- Hawkers, T. (1977) *Structuralism and Semiotics.* Berkeley: University of California Press.
- Hoffmeyer, J. (1996) *Sings of Meaning in the Universe.* Bloomington: Indiana University Press.
- Kothari, C. R. (2008) *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing Ltd.
- Kisarazo, K., Maguo, M., & Mahonge, F. (2025) “Ubainishaji wa kejeli zilizomo kwenye nyimbo za Taarab za Khadija Kopa,” katika *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili,* 8 (1), kur 1-16
- Ligembe, N. (1995) “The Use of Methaphor in Penina’s *Lina Ubani.*” M.A Dissertation, University of Dar es Salaam.
- Massoud, S. R. (2022) “Kuchunguza taswira katika nyimbo za taarab za Kimahaba za Khadija Kopa.” *Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*
- Mulokozi, M. M. (1996) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. na T. S. Y. Sengo (1995) *History of Kiswahili Poetry [AD 1000-2000].* Dar es Salaam: TUKI.
- Njogu, K. na Rocha, C. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.
- Omary, M. (2011) “Siasa katika Mashairi ya Euphrase Kezilahabi: Mifano kutoka Dhifa na Karibu Ndani,” *Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
- Safari, J. (2010) “Utangulizi katika Diwani ya Midulu.” Dar es Salaam: AERA.
- Sengo, T. S. Y. M. (1973a) “Mtu ni Utu (G. Mhina),” katika *Hisi Zetu,* Dar es Salaam: TUKI.

- Sengo, T. S. Y. M. (1973b) “Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii,” katika *Jarida la Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.
- Sengo, T. S. Y. M. (1987) *Fasihi Simulizi. Sekondari na Vyu*: Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.
- Sengo, T. S. Y. M. (2009) *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA
- Sengo, T. S. Y. M. (2010) *Diwani ya Midulu*. Dar es Salaam: AKADEMIYA
- Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi:
- Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.
- Wendo, F. & Titus, K. (2025) “Maudhui ya Ukungwi katika nyimbo teule za Taarab,” katika *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 8(2), kur. 119-132.

Disclaimer/Publisher’s Note: The statements, opinions, and data contained in all publications are solely those of the individual author(s) and contributor(s) and not of **AJHAS** and/or the editor(s). **AJHAS** and/or the editor(s) disclaim responsibility for any injury to people or property resulting from any ideas, methods, instructions, or products referred to in the content.